

Maana ya Mithali 29:9 Mwenye hekima akijadiliana na mpumbavu;  
Akikasirika au akicheka, pia hapana raha.

*Mithali 29:9 Mwenye hekima akijadiliana na mpumbavu;  
Akikasirika au akicheka, pia hapana raha.*

Mstari huo kwa lugha rahisi tunaweza kuuweka kwa namna hii.  
“Mwenye hekima akijadiliana na mpumbavu, akijibu kwa kicheko au  
kwa hasira, matokeo ni yaleyale tu hakuna amani au suluhisho”

Unafunua sifa za mpumbavu, kwamba sikuzote mwitikio wake wowote  
hauwezi kuleta mabadiliko. Kwamfano labda hoja imetolewa na  
ikamuumiza kiasi cha kumfanya ajibu kwa hasira. Sasa wewe waweza  
tarajia pengine jambo hilo limengusa kweli moyo, litambadilisha lakini  
matokeo yake ni kwamba anakuwa vilevile, Halikadhalika waweza kutoa  
hoja ikamfanyaacheke ukitarajia kitaambatana na badiliko lolote ndani  
yake lakini hakuna.

Maana yake mpumbavu, haguswi kwa ukali au kwa wepesi wa maneno  
ya aina yoyote...Na hivyo ni kuachana naye Tu.

Tukiachia wapumbavu wa kawaida tunaowafahamu..Mpumbavu hasaa ni

Maana ya Mithali 29:9 Mwenye hekima akijadiliana na mpumbavu;  
Akikasirika au akicheka, pia hapana raha.

yule mtu anayeikataa kweli ya Mungu mfano wa wale waandishi na mafarisayo wakati wa Bwana Yesu (Mathayo 23:17), mtu wa namna hii unapomuhubiri injili, hata imchomeje au imchekesheje hawezি kufikiri hata chembe kubadilika, kinyume Chake ni mapambano tu.

Bwana Yesu alitufundisha na kutuambia kuwa si kila mtu ni wa kumtupia lulu zetu, maana yake wanaweza kutugeukia na Kuturarua. Ukiona mtu anaishia kwenye ubishi tu na mashindano, ni kuachana naye na kugeukia waliotayari kupokea.

Bwana akubariki.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kubofya link hii >>

**<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>**

Kwa mawasiliano: +255693036618 au +255789001312

Maana ya Mithali 29:9 Mwenye hekima akijadiliana na mpumbavu;  
Akikasirika au akicheka, pia hapana raha.

Bwana akubariki.

### **Mafundisho mengine:**

*Mpumbavu ni nani katika biblia? (Zaburi 14:1, Mithali 10:14)*

*Elewa tafsiri ya Mithali 27:22 Hata ukimtwanga mpumbavu kwa  
mchi kinuni.*

*KILINDI CHAPIGIA KELELE KILINDI.*

Share on:  
WhatsApp